

Wakenya Waliosahauliwa: Waogiek Wanavyoathiriwa na Miradi ya Maendeleo

Na Nyang'ori Ohenjo

Jamii ya Ogiek, yenye idadi ya watu takriban 20,000, inaaminika kuwa ndio jamii kubwa zaidi kati ya jamii zilizosalia ambazo maisha yazo ya kiuchumi ni uwindaji na uchumaji wa vyakula katika misitu. Watu hawa tayari wamejitambulisha kama jamii asilia, ili haki zao zitambuliwe na kulindwa inavyostabili kulingana na sheria za kimataifa, na hasa kama inavyotambuliwa na Agano la Kimataifa la Shirika la Ijara nambari 169 Kifungu nambari 1 (b)¹, Umoja wa Mataifa, na vile vile Tume ya Haki za Watu na Jamii ya Afrika.

Kuna uwezekano mkubwa kwamba Ogiek ndio jamii asilia Afrika Mashariki na walipatikana nyanda za juu za maeneo ya misitu. Kulingana na Mzee Nagol: “Mababu wetu walituhadithia kuwa sisi tayari tulikuwa nchini humu kabla ya kuwasili makabila mengine”². Msimamo huu unaungwa mkono na watu wengine, kama vile G Yeoman, anayesema: “Hawa ni watu wa jadi katika maisha ya uwindaji na uchumaji wa vyakula mwituni...”³

Kwa wakati huu, Waogiek wanapatikana katika miinuko ya Mau na Aberdare mkoani Bonde la Ufa, na pia katika maeneo machache ya Mlima Elgon magharibi mwa Kenya. Ukoo, ambao ulijumuishwa na makundi madogo madogo kadhaa, ndio hushughulikia mambo ya ardhi, na ndio taasisi muhimu zaidi katika jamii ya Ogiek. Ogiek, hata hivyo hawajawahi kufahamika kuwa na mipangilio mahsusni ya kisiasa kama vile uchifu ama mabaraza ya uongozi.

Ripoti hii inaangazia kuhamishwa Waogiek kutoka ardhi yao, jambo ambalo limepelekea kukosa kwao maendeleo na pia kuwa tishio kwa mila na desturi zao.

Haki za jamii asilia katika muktadha wa maendeleo

Wadorobo hawa [Yaani Waogiek] wamepeperushwa kama takataka na upepo wa maendeleo ... inabidi sasa tupendekeze watengewe mahali maalum pa kukaa.”⁴

Hukumu hii ya Tume ya Ardhi Ya Carter⁵ (1932, ukurasa wa 8) inatoa taswira bora ya vile Waogiek wamekandamizwa miaka ya hapo awali hadi sasa. Tume hii iliishia kupendekeza kuwa Waogiek waondolewe walipokuwa wakiishi, sehemu zilizohitajika na wakoloni kuendeleza ukulima, na kutengewa nafasi karibu na makabila mengine, kuwezesha usilimishaji. Hata hivyo, ingawaje Waogiek walionekana kama wasiopenda maendeleo, wao walitaka maendeleo kulingana na hali yao ya maisha anavyoelezea Mzee Kaliasoi Chesimet wa Tinet: “Wageni waliokuja waliikata misitu na kuanzisha mashamba ya Majani Chai na Maua.

Hata hivyo, sisi tumekuwa tukisisitiza kwamba hatutaki maendeleo ya kushurutishwa yasiyotufaa, bali tuachwe tuyaendeleze maisha yetu kwa njia ambayo kwetu ni mufti.”

Tangu enzi za ukoloni, Waogiek wamehamishwa kutoka makao yao ya jadi bila mashauriano, kibali chao, au hata kulipwa fidia kwa ardhi waliyoiipoteza. Kwa muda huu wote, hawajajumuishwa kwa njia yo yote ile katika mipango na miradi ya maendeleo isipokuwa kusukumwa kwenye ardhi isiyowafaa. Joseph Towett⁶ analalamika: “Inasemekana kuwa hatutaki maendeleo. Lakini swali ni kwamba, maendeleo haya ni yepi na ya wapi.” Swala hili la maendeleo linapata nguvu ikizingatiwa kuwa watetezi wa haki za binaadamu wamaeonya kuwa maendeleo huenda yakawa chanzo cha kuyaangamiza makabila.⁷

Ustaarabu wa Waogiek ndio nguzo yao. Kulingana na Bi Rael Kibilo kutoka eneo la msitu wa Tinnet: “Kabla misitu yetu kukatwa, tulikuwa na ustaarabu wetu na tamaduni zetu... na ye yote anayeiangamiza misitu hii bila shaka anauangamiza ustaarabu wetu.” Uhamishwaji wa Waogiek kutoka maeneo yao, ambayo ni madhabahu kwao, kunapelekea kupotea ustaarabu wa watu hawa na vile vile kunakiuka sheria za kimataifa za haki za binaadamu, nyinginezo ambazo taifa hili limeidhinisha (Kwa mfano, Kifungu nambari 15 cha Agano la Kimataifa la Haki za Kiuchumi, Kijamii na Ustaarabu, ambalo Kenya imeidhinisha).

Serikali inaithibiti ardhi ya Waogiek kupitia sheria tatu: Sheria ya ardhi za Serikali ya mwaka 1970, iliyorekebisha mwaka 1986, Sheria ya Misitu ya 1957 na kurekebisha 1964, na Sheria ya Wanyama wa Pori (1977 iliyorekebisha 1985).

Ardhi ya Waogiek inaainishwa na serikali ama kama misitu ya serikali au mbuga za wanyama wa pori. Serikali haihitajiki kuwashauri Waogiek, ama ye yote yule, kabla ya kuchukua uamuzi wa kutaifisha ardhi yo yote kulingana na sheria zilizoko.

Ukataji miti ni moja ya sababu nyingi za uharibifu wa maeneo ya misitu wanamopatikana Waogiek, hasa kuanzia miaka ya 90. Kampuni tatu, Pan African Paper Mills, Raiply Timber na Timsales Limited zimepatiwa vibali vya kukata miti kutoka sehemu hizi kutokana na tetesi kuwa Raiply na Timsales zimewaajiri zaidi ya Wakenya 30,000 ilihali serikali ina hisa katika kampuni ya Pan African Paper Mills⁸.

Ardhi ya Waogiek hali kadhalika imechukuliwa na kugawiwa watu binafsi, watu ambao inaaminika wana ushawishi mkubwa kisiasa, huku ikielezwa kuwa ardhi iliyotwaliwa inapewa watu wasio na makao. Kutwaliwa ardhi kumekuwa kukiendelea tangu 1932. Kati ya miaka ya 1963 na 1971, takriban heka 48,000 za ardhi zilitwaliwa na serikali kwa kutumia sheria ya misitu.

Miradi ya maendeleo vile vile imechangia kupotea kwa ardhi ya Waogiek, kama vile Eneo la Wanyama Pori Mlima Elgon, mradi ulioanzishwa miaka ya 80 na kufanywa Mbuga ya kitaifa ya Wanyama Pori ya Mlima Elgon mwaka 1992.

Watu binafsi aidha wamenyakua ardhi hii na kuendeleza ukulima wa majani chai, pareto na maua. Ukuzaji wa pareto unaathiri sana uzalishaji asali kwa vile nyuki wengi hufa kutokana na sumu ipatikanayo katika pareto.

Mambo haya yakizingatiwa, ni rahisi kuelewa ni kwa nini zaidi ya Waogiek asilimia 95 ni fukara, hasa hali hii ikichunguzwa katika muktadha wa ufafanuzi wa Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Ustaarabu. Kamati hii inaeleza kuwa umaskini hutokana na watu kunyimwa matumizi ya mali yao asili kwa kubaguliwa kikabila au kidini⁹.

Athari ya kupoteza Ardhi

Umaskini uliokithiri ndio athari kubwa inayotokana na kupoteza ardhi kwa Waogiek. Umaskini huu umepelekea kuwepo hali duni ya masomo, na hali mbaya ya afya: wanawake wameathiriwa zaidi kwani kitamaduni hawana haki ya umilikaji mali na hivyo huishia kuwa maskini zaidi. Utafiti uliofanikisha ripoti ulithibitisha kuwa zaidi ya asilimia 95 ya Waogiek hawawezi kujimudu kupata lishe bora mara moja kwa siku¹⁰.

Waogiek wamepoteza uchumi wao wa kitamaduni, na wamelazimika kuingilia ukulima. Hata hivyo, hawana ustadi wa ukulima na vile vile maeneo yao hayafai kwa kilimo cha vyakula, hali zinazowapelekea kupata mazao duni. Isitoshe, mara nyingi wananyaswa wanapowauzia wanabiashara wa kati bidhaa zao¹¹.

Asali ni mojawapo ya bidhaa ambazo Waogiek wanazozalisha, bidhaa ambayo ikiendelezwa, inaweza kuchangia pakubwa katika kupunguza umaskini katika jamii hii, hasa asali hiyo ikitengenezwa kwao¹². Kwa hivi sasa, uzalishaji wa asali unaathiriwa na uchomaji makaa na vile vile ukulima wa pareto: uchomaji makaa una athari maradufu kwani pamoja na kuharibu misitu, pia nyuki huuwawa na moshi unaotokana na uchomaji huu.

Umaskini katika jamii ya Ogiek umepelekea kuwepo idadi ya juu ya watu ambao hawajui kusoma na kuandika (zaidi ya asilimia 80) kwani wazazi hawajimudu kifedha kuwapeleka watoto wao shuleni¹³.

Wasichana wanaathirika zaidi, hali inayopelekea wengi wao kuolewa wangali wabichi. Hivi karibuni, ukahaba umeibuka katika jamii hii kwani wasichana wengi wamejipata wazazi nje ya ndoa bila ya uwezo wa kujitunza wao na watoto wao. Hali hii imepelekea kuenea kwa magonjwa ya zinaa kama vile ukimwi na hivyo, kuathiri maisha ya jamii nzima kwa njia mbali mbali.

Shule za msingi ni chache na aghalabu zinapatikana mbali na makao ya Waogiek, ilihali hakuna shule yo yote ya upili katika maeneo wanamoishi Waogiek. Watoto wanaofuzu mitihani ya shule za msingi, kwa hivyo, huhitajika kwenda shule za mabweni mbali na kwao. Kwa sababu hii, na pia kwa kuwa pesa ni haba, watoto wengi hawatamatishi masomo yao ya shule za upili.

Kutokana na kuzuiliwa kuchuma madawa ya kienyeji, na aidha kwa vile wengi wao hawana pesa za kulipia matibabu hospitalini, ambazo aghalabu ziko mbali, hali ya afya ya Waogiek imeathirika vibaya mno. Kwa hivi sasa, katika eneo la Mau, kuna daktari mmoja kwa kila watu zaidi ya 6,000 jambo ambalo haliwawezeshi wengi wa Waogiek kupata matibabu inapohitajika. Kaliasoi Chesimet anaeleza: “Misitu ndio hospitali yetu, na ndimo mna madawa yetu.”

Kutokana na umaskini, na pia kwa vile Waogiek hawawezi kupata madawa ya kienyezi, maisha ya Waogiek yamepelekewa kwa wastani kuwa mafupi. Utafiti iliofanikisha ripoti hii ulibainisha kuwa maisha ya wastani ya Waogiek ni miaka 46, na kati ya watoto kumi, watano hufa kabla ya kufikisha miaka mitano

Uharibifu wa Mazingira

Uharibifu wa misitu katika maeneo wanamoishi Waogiek hakuwaathiri tu watu wa jamii hii, bali pia ni tatizo kwa nchi nzima ya Kenya. Nchi hii inahitaji asilimia 10 ya ardhi ya misitu, ili ipate maji ya kujitoshleza lakini ina asilima 1.7 pekee. Kenya inategemea maji yatokako maeneo yenye misitu, huku maeneo ya Mlima Elgon na miinuko ya Mau ikigharimia zaidi ya asilimia 50¹⁴.

Jamii asilia zinatambuliwa kuwa na uwezo mkubwa wa kuhifadhi mazingira yao na jamii ya kimataifa¹⁵. “Jamii hizi ni hifadhi ya hekima ya kitamaduni ... Kutoweka kwao ni pigo kwa jamii yote inayoweza kujifunza mengi kuhusu vile ya kuhifadhi mazingira,” inaeleza ripoti *Our Common Future* ya mwaka 1987, iliyoandikwa na Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Mazingira na Maendeleo¹⁶. Kwa kuendeleza kuharibiwa kwa misitu, kwa hivyo, serikali ya Kenya inakiuka desturi za kuwezesha maendeleo stahimili.

Matumizi ya maeneo ya miinuko ya Mau, Aberdare na Mlima Elgon na jamii ya Ogiek ni muhimu. Hivi ni kwa sababu maisha yao ya kitamaduni ya uwindaji na uchumaji hayaathiri mazingira. Kama anavyosema Kaliasoi Chesimet: “Tulipotaka mnyama, tuliua mmjao tu.” Vile vile, katika jamii hii, kila ukoo ulipewa mnyama kumlinda kutokana na desturi ijulikanayo kama *totem*, kwa hivyo, mnyama huyo hawezi kuwindwa na watu wa ukoo huo husika. Aidha, uzalishaji wa asali ulichangia pakubwa kuhakikisha kuwa misitu ilendelea kunawiri kutokana na nyuki kutawanya mbegu za uzazi za mimea ikiwemo miti. Mwisho, kutokana na hali kuwa madawa ya Waogiek yalipatikana mwituni, walikuwa hawana budi kuulinda misitu hii.

Hekima ya kitamaduni ya mazingira hupatikana kutokana na maingiliano ya binadamu na mazingira yao, hivi kwamba kuwahamisha Waogiek kutoka ardhi yao ya jadi kutavunja desturi ya kupokezwa elimu hii kizazi kimoja toka kingine. Uchumaji wa vyakula na madawa ilikuwa ni kazi ya wanawake na watoto; wanawake nao walihitajika kuiendeleza elimu hii kwa vizazi vilivyofuata ili pasiwe na pengo. Uhifadhi wa utajiri wa elimu hii ya kitamaduni, kwa hivyo, utategemea pakubwa watu wa jamii hii kuendelea kuyatumia maeneo ya ardhi yao ya jadi kujiendeleza kimaisha.

Mapambano ya Waogiek

Kwa sababu ya kudhalilishwa haki zao za ardhi, Waogiek, kuanzia majukwaa ya kimataifa hadi kitaifa, wamejaribu kwa vyo vyote vile ili kupigania haki zao. Wamekuwa wakijizatiti kuzuilia kunyakuliwa zaidi kwa ardhi yao na kujaribu kupata umiliki tena wa ile ardhi iliyonyakuliwa¹⁷.

Kimataifa, Waogiek wamewakilishwa na mashirika yao katika mikutano kama vile Mkutano wa Kimataifa wa Maendeleo Stahimili uliofanyika Johannesburg, Afrika Kusini, mwaka 2002, Mkutano wa Ulimwengu wa kupambana na Ubaguzi uliofanyika Durban, Afrika Kusini, mwaka 2001, na Kongamano la Umoja wa Mataifa la Jamii Asilia. Kwingineko, wamewakilishwa na mashirika mengine ya haki za binadamu katika mikutano kama vile Kongamano la Umoja wa Mataifa la Jamii Chochole.

Kitaifa, Waogiek wamefanya maandamano, wamewasilisha kesi mahakamani, na vile vile wameshiriki katika mifanyiko ya urekebishaji wa sheria za ardhi na vile vile urekebishaji wa katiba ya Kenya.

Kati ya haya yote, ni juhudi zao za kutumia mahakama ambazo zimekuwa za kuvunja moyo. Katika uamuzi wa mahakama wa tarehe 15 Machi 2000 kwa mfano, majaji wawili wa Mahakama Kuu walisema kuwa Waogiek walikuwa wametupilia mbali tamaduni zao na kwa hivyo kupoteza haki zao za ardhi yao ya jadi.

Kwa hivi sasa, Waogiek wanaamini kwamba ni katiba mpya tu ambayo itasuluhisha matatizo yao, kwa kuzilinda haki zao kama jamii asilia. Anavyosema mnyeje Kilisha Lekwenan, aliye na umri wa miaka 102, Wakenya hawana budi kutunga katiba ambayo itaziwezesha jamii tofauti za humu nchini kuishi katika hali ya

kuheshimiana na utangamano. Akibashiri kuwa hatawahi kunufaika na zao la Tume ya Urekebishaji Katiba, anatoa wito hata hivyo, kuwa urekebishaji katiba ni jambo lililohitajika kwa vyo vyo vile ili ukandamizwaji jamii mbali mbali usitishwe.

Marejeleo

- 1 Kifungu 1(b) (*ILO Convention 169 on Indigenous and Tribal Peoples*) kinazitambua jamii asilia kama: "Jamii zilizomo mataifa huru ambazo zilikuwemo nchini humo, kabla ya ukoloni na ambazo zimehifadhi na kuendeleza desturi zao kisiasa, kichumi na kijamii."
- 2 Nukuu zote zilizomo humu zinatokana na utafiti wa CEMIRIDE (Nyang'ori Ohenjo) 2002, na mahojiano kati ya Survival International (Virginia Luling) na Wazee wa Ogiek kule Tinet 2002.
- 3 Yeoman. G., 'High Altitude Forest Conservation in Relation to the Dorobo,' *Kenya Past and Present*, Vol 3 1933.
- 4 *Dorobo* ni jina la utani walilopatiwa Waogiek na Wamaasai kwani hawakumiliki mifugo. Jina hili huashiria watu *maskini hohehahe*.
- 5 Tume ya Carter ilituniwa mwaka wa 1932 na Waziri wa nchi zilizokoloniwa ili kuchunguza mahitaji ya ardhi ya Waafrika nchini Kenya.
- 6 Joseph Towett ni mmoja wa viongozi wa Ogiek anayeongoza shirika la Ogiek Welfare Council (OWC). Mashirika mengine ni Ogiek Intergrated Rural Project (ORIP), Ogiek Peoples Development Program(OPDP), Chepkitale Indigenous Peoples Trust (CIPT) na ODECECO.
- 7 Stavenhagen. R., *The Ethnic Question*, Tokyo, United Nations University Press, 1990. Anasema kuwa kuangamizwa jamii (Ethnocide) hutokea pale ambapo jamii au kabila linapoteza unafsi wake na hutokana na athari za miradi za maendeleo ya kitaifa.
- 8 Astill, J., 'Tribal Trials,' *The Gurdian*, tarehe 13 Machi 2002 ukurasa 8.
- 9 UN Doc. E/C.12/2001/10;10 Mei 2001, aya ya 11
- 10 Utafiti wa CEMIRIDE kwa niaba ya Mradi wa Maendeleo na Wachochole wa Minority Rights Group.
- 11 *Traditional Occupations of Indigenous and Tribal Peoples: Emerging Trends*, ILO, 2000, Ukurasa 80
- 12 Miradi ya uzalishaji asali ya serikali iliyopelekwa Busia na Mkoa wa Nyanza, na vile vile Ukambani Mkoani Mashariki ilitumbukia nyongo kwani jamii hizi hazikuwa na ustadi wa kazi hii.
- 13 Kati ya idadi ya watu takriban 20,000, Waogiek wana chini ya watu watano waliofuzu vyeti vya digrii kutoka vyuo vikuu.
- 14 [Gazeti la Daily Nation](#) la Machi 10 liliwanukuu wataalamu wa mazingira wakionya kuwa kuendelea kuharibiwa misitu hasa katika maeneo ya Aberdare na Mau kutaathiri upatikanaji wa maji ya kutosha nchini humu. (www.nationaudio.com)
- 15 Mkutano wa Kimataifa wa Maendeleo Stahinili (*World Summit on Sustainable Development*) uliofanyika Afrika Kusini ulizitambua jamii asilia kuwa kigezo muhimu katika harakati za kufanikisha maendeleo stahimili. Rejelea pia Ripoti ya United Nations Development Programme (UNDP), *The UNDP Human Development Report 2000*.
- 16 [Tume ya Ulimwengu ya Mazingira na Maendeleo](#), (*World Commission on Environment and Development*), *Our Common Future*, Oxford, Oxford University Press, 1987 (www.doc.mmu.ac.uk/aric/cae/Sustainability/Older/Brundtland_Report.html)
- 17 www.ogiek.org/report

page 4

Tunatetea kutambuliwa haki za wachochole na jamii asilia

Mapendekezo

Kwa Serikali ya Kenya:

- Serikali ya Kenya inafaa ihakikishe kuwa Katiba mpya imeandikwa na kutekelezwa haraka iwezekanavyo. Katiba hii inafaa izitambue jamii asilia za Kenya, pamoja na haki zao za unafsi wao na umiliki wa ardhi zao za jadi kulindwa. Aidha katiba hii inafaa kutambua haki ya watu wa Ogiek kulipwa fidia ya ardhi ambayo wameipoteza hadi sasa.
- Serikali ya Kenya inafaa kutekeleza majukumu yake ya kitaifa yanayozihusu jamii asilia. Serikali inahitajika, hasa, kuidhinisha na kutekeleza Agano la Kimataifa la Jamii Asilia nambari 169 la Shirika la Kimataifa la Ijara (ILO).
- Haki za binadamu za jamii asilia inafaa zizingatiwe katika sera za, mipango na miradi ya, maendeleo. Waogiek vile vile wanafaa kushauriwa kuhusu mipango ya maendeleo ya usoni ambayo ina uwezo wa kuwaathiri.

- Leseni zote ambazo zimepewa kampuni kukata miti katika maeneo manamopatikana Waogiek zinafaa kufutuiliwa mbali.
- Serikali ya Kenya inafaa kutoa hesabu kamili ya jamii asilia katika muktadha wa vigezo vya kuthibitisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii, ili kubainisha viwango vya maendeleo katika jamii hizi, na hapo kutambua matakwa ya jamii hizi makubwa.

Kwa Jamii ya Kimataifa

- Jamii ya kimataifa (Wafadhili, Mashirika ya Maendeleo, Mashirika ya Kimataifa yasiyo ya Serikali, na Mashirika ya Umoja wa Mataifa) inayowakilishwa nchini Kenya inaombwa kuwa ihakikishe kuwa inazingatia haki za binadamu za jamii asilia katika miradi yao ya maendeleo katika maeneo yanamopatikana jamii hizi. Hasa, jamii hii inafaa kuhakikisha kuwa Waogiek wameshauriwa kabla mradi wo wote haujaidhinishwa.
- Jamii ya kimataifa inafaa kuangazia kuwaelimisha Waogiek, na hasa wanawake, ili waweze kujimudu katika kuzitetea haki zao kitaifa na kimataifa.
- Jamii ya kimataifa, pamoja na serikali ya Kenya, inafaa kuunda tume itakayochunguza makosa ya kukiukwa haki za Waogiek, na hasa kunyang'anywa ardhi yao. Tume hii, katika muda usio mrefu, itahitajika ichapishe ripoti yake, yakiwemo mapendekezo yake, yanayofaa kuzingatia swala la iwapo jamii hii inafaa kurudishiwa ardhi yake ya jadi au kulipwa fidia.

Xxxxxxx

Mradi wa Wachochole katika Maendeleo wa *Minority Rights Group International* huzingatia utafiti na utetezi wa haki za wachochole, kwa madhumuni ya kutathmini miradi ya maendeleo inayaowabagua wachochole na watu kutoka kwenye jamii asilia, na ulibuniwa na shirika la *Minority Rights Group Internatioal* na Washirika wake.

Shukrani MRG na Washirika wake wa miradi wangependa kutoa shukrani zao kwa misaada ya kifedha kutoka kwa Christian Aid, Cordaid, DFID, Serikali ya Norway, na Staples Trust. Ripoti hii iliandikwa kwa lugha ya Kiingereza na kutafsiriwa na Nyang'ori Ohenjo, afisa wa miradi ya utetezi na habari wa CEMIRIDE. Waliouelekeza mradi: Angela Haynes (MRG) na Korir Sing'oei (CEMIRIDE); Mhariri: Sophie Richmond.

Wakenya Waliosahauliwa: Waogiek Wanavyoathiriwa na Miradi ya Maendeleo © Minority Rights Group International, Uingereza, na Centre for Minority Rights Development (CEMIRIDE), Kenya, Januari 2003. Ripoti hii imechapishwa kama mchango katika kuendeleza elimu jamii na ni moja kati ya miradi ya Mradi wa Wachochole katika Maendeleo wa MRG. Ripoti hii haimaanishi kuwa haya ni maelezo ya kina kuhusu msimamo wa MRG ama washirika wake.

Minority Rights Group International ni shirika la kimataifa lisilo la serikali ambalo kazi yake ni kuwezesha haki za wachochole na jamii asilia kutambulika na kulindwa ulimwenguni kote. Shughuli zetu zinazingatia utetezi wa haki za binadamu kimatifa, kutoa mafunzo, uchapishaji na kuwafikia watu na jamii. Kazi zetu zinaelekezwa na mapendekezo na mahitaji ya washirika wetu wanaowakilisha wachochole na jamii asilia. MRG ni shirika ambalo limetunukiwa hadhi ya Ushauri na ECOSOC. MRG limesajiliwa kama shirika fadhili nambari 282305 na pia kama kampuni binafsi Uingereza nambari 1544957. CEMIRIDE ni shirika la kitaifa la utafiti na utetezi wa haki za binadamu za wachochole na jamii asilia, ili kufanikisha kutambuliwa, keheshimiwa na kulindwa kwa haki za watu hawa, na kuendeleza utangamano kati ya jamii tofauti za Kenya. Shirika hili limesajiliwa kama inavyohitajika na sheria ya usajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali ya Kenya nambari OP.218/051/2002/0149/2240

Centre for Minority Rights Development,
Sanduku la Posta 14692,
00100 Nairobi.
Nambari ya Simu: +254 (0) 2 500 521
Kipepesi: +254 (0) 2 248 214
Anwani ya barua pepe: cemiride@hotmail.com

Kitandao: www.cemiride.org

Minority Rights Group International,
379 Brixton Road,
London, SW9 7DE.
Nambari ya Simu: +44 (0) 20 7978 9498
Kipepesi: +44 (0) 20 7738 6265
Anwani ya barua pepe: minority.rights@mrgmail.org
[Kitandao: www.minorityrights.org](http://www.minorityrights.org)

Picture Caption translated:

Waogiek wakiwa mahakamani kusikiza moja ya kesi zao.